
# KUZUIA MCHWA BILA KEMIKALI



**HDRA – Kwa huduma za Kilimo - hai**

Termite control without chemicals

**Mchwa ni Nini?**

Mchwa ni kati ya jamii ya wadudu (*Isoptera*) wanaojumuisha zaidi ya takribani 2500. Kati yao 300 ni waharibifu. Katika nchi za hari (*tropics*) mchwa ni baadhi ya wadudu walio waharibifu kwa kilimo, mwitu na nyumba.

Kuna jamii ndogo na kubwa zinazopatikana chini ya ardhi, kwenye sehemu za mwituni katika miti iliyozeeka au yenye shina la shimo, na baadhi hujenga kalibu nakshi (vichuguu).

Kabla ya kuzuia mchwa, sharti ufahamu aina ya jamii. Hii hutambuliwa kwa kutazama aina ya uharibifu uliotokea kwenye miti au mimea.

Aina ya mchwa wasumbufu ni wale wanaoshambulia mabaki ya mimea, rutuba na boji-ezefu. Hatahivyo, iwapo chakula hiki kitakosa, basi itawabidi kuharibu mimea kama vile njugu, mtama na mahindi.

Aina ya mchwa wa mavuno hupatikana katika sehemu kame na zile zisizotumika kwa kikamilifu. Mchwa hawa hujenga kalibu nakshi chini ya ardhi. Kalibu hizi haziwezi kutambuliwa kwa urahisi. Aina ya mchwa hawa hukusanya mimea michanga, nyasi au mimea iliyodhoofika.

**Je, Mchwa wana faida?**

Ijapokuwa mchwa wamejulikana kama wadudu waharibifu, kwa uchache wanaweza kuwa na faida. Kabla ya kuwazuia ni bora kutafakari yafuatayo.

Faida ni kama:

- Kueneza hewa kwenye mchanga.
- Kuimarisha rutuba kutokana na kinyesi chao.
- Kuimarisha umbo na rutuba ya mchanga wanapojenga kalibu nakshi zilizo na madini.
- Kalibu nakshi hujumuisha madini muhimu kwa mifugo inapolambwa.
- Mchwa ni chakula kilicho na proteni kwa kuku na wanyama wengine na hata binadamu.

**Matumizi ya kemikali**

Tangu jadi, njia ya kuzuia mchwa ni matumizi ya dawa za kisanisia zenye kemikali. Aidha madawa hayo ni ghali na yenye madhara mengi.

**Usalama kwa Binadamu**

Madawa yenye sumu huenea hadi kwenye mikondo ya maji au kufanya chimbuko kwenye vyakula. Hii ni hatari kwa binadamu. Wakati mwingi madawa hayo yanaweza kuwa na maagizo yasiyoeleweka au yaliyoandikwa kwa lugha isiyofahamika. Jambo hili limezua maaafa na hata kusababisha vifo.

**Usalama kwa mazingira**

Madawa ya kemikali yanahatari kwenye mazingira. Baadhi ya madhara ni kama yafuatayo:

- Madawa ya kisanisia yanaweza kuwaua wadudu wenye manufaa.
- Madhara yaweza kusalia kwenye mazingira na kusababisha matatizo katika miaka ya baadaye.
- Wadudu huimarisha nguvu za kinga dhidi ya madawa hayo na kuwafanya sugu. Jambo hili hupelekea kutengenezwa madawa yenye nguvu zaidi.

**Gharama**

Matumizi ya dawa au njia za kiasili ni rahisi pasipo gharama kubwa. Viungo vinavyo hitajika hupatikana shambani.

**Njia za kiasili za kuzuia Mchwa**

Kuna njia nyingi za kuzuia mchwa pasipo kutumia madawa ya kisanisia yenye kemikali. Njia hizi hufanya kazi katika mandhari ya kawaida.


- Njia ya kiasili au hai, haina madhara kwenye mazingira na haitawadhuru wadudu wenye manufaa au watu wanaotumia.
- Njia ya kiasili daima hutumia viungo vipatikanavyo shambani wala sio viungo vya kuagiza.
- Njia ya kiasili ni rahisi kutumia.
- Njia ya kiasili huimarisha uwiano wa kimandhari na nasaba ya kizazi (tabia ya urithi) katika kilimo ili kuzuia wadudu waharibifu.
- Njia ya kiasili **huzuia** tuu, bali sio kuangamiza mchwa.

Hali ya kuzuia hutegemea aina ya jamii ya wadudu, miti au mimea, hali ya hewa na aina ya mazingira. Halikadhalika aina ya mchanga.

Njia za kuzuia mchwa zilizoko kwenye kitabu hiki zimetokana na uchunguzi wa kibinafsi na haijabainika au kukadiriwa kwa wingi.

**Kuongeza boji kwenye mchanga**

Baadhi ya mchwa hutegemea mabaki ya mimea. Iwapo sehemu haina boji au mabaki ya mimea, basi mchwa huvamia mimea iliyo hai. Kuzuia haya ni bora kupanda boji la kijani au kuongeza boji kwenye mchanga.



*Kuongeza boji kwenye mchanga ili kuzidisha kiwango cha viungo asili.*

**Kuendeleza mahasimu wa mchwa**

Kuna aina nyingi ya wanyama na wadudu wanaohisimu mchwa. Baadhi ya wadudu hao ni buibui, jamii ya mende, siafu na nyigu. Mahasimu wengine ni chura, mjusi, ndege na wanyama wengine kama *aardvarks,* popo, kima na binadamu. Kuendeleza juhudi za mahasimu hawa kutapelekea kupungua kwa idadi ya mchwa. Miti ni muhimu sana na hufanya ngome ya baadhi ya mahasimu waliotajwa hapo juu. Ni bora basi kuhifadhi na kuitunza miti.

**Kubadilisha aina ya viungo**

Iwapo utafahamu aina ya viungo vinavyo vamiwa na mchwa, ni bora kubadilisha. Kwa wakati wowote jaribu kuzuia kuwacha mimea bila boji.

Njia isiyodumu ni hali ya kuwapatia mchwa chakula kingine kama boji-ezefu ili wasivamie mimea yako. Katika Uganda na Afrika Kusini boji-ezefu linalotokana kwa machujo ya mbao, mabaki ya mahindi na jivu, huzuia mchwa kuvamia mimea. Mchwa huvutiwa na boji-ezefu bali sio mimea. Aidha aina ya nyasi ya *vetiver grass* (*Vetiveria zizanioides*) huzuia mchwa kuvamia miti.

Hatahivyo, kubadili chakula au matumizi ya boji-ezefu yaweza kuzidisha idadi ya mchwa. Hii hutegemea tuu aina ya jamii ya mchwa au aina ya miti au mimea unayokuza.

**Mzunguko wa mimea**

Rutuba ya mchanga hudhoofika iwapo mkulima atapanda aina moja ya mimea msimu baada ya msimu miaka nenda rudi. Mimea katika sehemu kama hiyo hudhoofika na kuvamiwa na mchwa. Mzunguko wa mimea waweza kuzuia matatizo haya.

Mzunguko wa mimea ni mfumo ambao aina tofauti ya mimea hukuzwa katika eneo fulani kila msimu kwa mwaka. Njia hii huimarisha umbo la mchanga na rutuba. Aidha wadudu na magonjwa huangamizwa.

**Kuatika mimea yenye afya**

¤ Mimea iliyodhoofu kwa kukosa maji, madini au yenye magonjwa, huvamiwa kwa urahisi na mchwa. Ni bora kuhakikisha afya ya mimea na kuipatia maji ya kutosha.

¤ Katika sehemu kame, ni bora kupanda wakati wa mwanzo wa msimu wa mvua ili mimea iweze kupata maji ya kutosha.

¤ Wakati wa kuatika, ni bora kuchagua mimea yenye afya. Chukua tahadhari wakati unapoatika mimea na kufyeka, kwani magofu hutokea na mchwa hushambulia sehemu kama hizo.

¤ Iwapo miche imepandwa kwenye vifuko, vifuko huzuia mchwa ila tuu visizuie mizizi. Hatahivyo, vifuko vya migomba ya ndizi huvutia mchwa.

¤ Ongeza boji kwenye sehemu utakayoatiki mimea. Usitumie mbolea ya kisanisia, kwani husababisha mimea kukua kwa haraka pasipo shina la nguvu kuhimili mchwa.

**Sumaku**

Unapoweka sumaku katika sehemu yenye vigutu au kalibu nakshi za mchwa, huzuia mchwa kuendeleza vichuguu hivyo. Hii hutatiza jamii ya mchwa wanaozingatia ujenzi wa kalibu nakshi katika muelekeo wa kusini-kaskazini mwa sumaku au magnetisi.

**Kuharibu kalibu na kuondoa malkia**

Sehemu zinazoporomoka udongo huzuia mchwa kujenga kalibu nakshi kubwa. Katika sehemu nyingine, kuvunjilia mbali kwa vigutu hivi huzuia ujenzi zaidi. Kulima mara kwa mara na kuharibu himaya ya mchwa huchangia sana katika kuzuia mchwa. Matokeo bora ni pale unapofikia malkia na kumuangamiza.

**Vizingiti**

Ujenzi wa vizingiti katika nyumba na bustani huzuia mchwa. Viungo vya kujenga vizingiti visiwe vile vinavyoweza kuvamiwa na mchwa. Halikadhalika viungo hivyo visichukuliwe kwa urahisi na mchwa.

## Mimea yenye uwezo wa kuzuia mchwa

### Mimea

Ufahamu ni haba kuhusu aina ya mimea iliyo na uwezo wa kukabili mchwa. Mimea ya kiasili ina uwezo kuliko ile ya kigeni. Katika Afrika mtama na mawele huhimili mchwa kuliko mahindi na kunde. Njugu ya kawaida huvamiwa kwa urahisi ukilinganisha na njugu ya bambara. Mimea mingi huvamiwa wakati wa mavuno au wakati wa kiangazi.

### Miti

Kiwango cha kuhimili mchwa hutegemea aina ya mti, umri wa mti, jamii ya mchwa na mahali unapopatikana (sehemu/nchi). Hatahivyo, kama mimea, aina ya miti ya kiasili ni bora kuliko ile ya kigeni. Ifuatayo ni orodha ya miti na mimea inayoweza kuzuia mchwa.

*Miti na Mimea inayoweza kuzuia Mchwa*

| Jamii | Jina la kawaida | Sehemu inayotumiwa kuzuia | Mawaidha |
|---|---|---|---|
| Acacia polyacantha | Mkengewa, Oyongo, Kivovoa or falcons claw (hook thorn) | | Nguvu nyingi kutoka kwa resin |
| Afromosia laxiflora | | Majimaji ya mgomba | |
| Albizia odoratissima | (black siris, fragrant albizia, tes shade tree) | Majimaji ya mgomba | |
| Albizia zygia | Nongo, oturbam | | Huzuia tuu bali sio kuangamiza |
| Azadirachta indica | Mkilifi, Mwarubaini, Mwarubaini kamili (neem, nim) | | |
| Borassus aethiopum | Mchapa, Mvomo, Mtappa, Murifate (African fan palm) | | Nyuzinyuzi zake ni dhabiti |
| Brachylaena hutchinsii | Mugugu, Kipungupungu, Muhuhu (muhugu oil tree) | | Mti mgumu na hauwezi kushambuliwa |
| Capparis aphylla | Mpapura chui, Mbadapaka, Mzezagunga, Shikumbu | Majimaji ya mbao | Huzuia mchwa |
| Catalpa bignonioides | (Indian bean tree) | | Huzuia Reticulitermes flavipes |
| Cedrusdeodora | (Himalayan cedar) | Majimaji ya mti | |
| Daniellia oliveri | | Gundi | |
| Detarium senegalense | | Majimaji ya mti | Sumu kuliwa |
| Dodonaea viscosa | Mkapwani (purple hop bush) | Majimaji ya mgomba | Kuhimili mchwa |
| Erythropleum suaveolens | Missanda, Mkelekele, Mbaraka-mkuu (Ordeal tree) | Majimaji ya mti | Sumu |
| Eucalyptus microcorys | | | Nguvu imara |
| Grevillea robusta | Umweyo, Umtisandugu (silky oak, silver oak) | | Maarufu nchini Tanzania |
| Juniperus procera | (E African pencil cedar) | | Nguvu dhabiti |
| Melia azedarach | Mmelia, Mwarubaini nusu (chinaberry, Persian lilac) | Majimaji ya matawi na mbegu | Sumu kali |
| Strychnos nux-vomica | | Majani | Sumu kali |
| Zanthoxylum Xanthoxyloides | Mjafari, Simbari, Ichunguluzi, Muvu | Majimaji | |

Kuna aina nyingine ya miti iliyo na uwezo wa kukabili mchwa mfano: *Acacia catechu*, *Acacia mearnsii* (Muwati, Mwati), *Acacia melanoxylon*, *Albizia saman*, *Afzelia cuanzensis* (Mbambakofi), *Balanites aegyptiaca* (Kilului, Olngoswa), *Bridelia micrantha* (Shikangania, Mutarakaranga, Umuronda-ng'ombe, Mitserie), *Cassia brewsteeri*, *Casuarina cunninghammiana* (Mvinje), *Eucalyptus camaldulensis* (Mkaratusi), *Gliricidia sepium*, *Grevillea glauca*, *Leucaena leucocephala* (Lusina, Mlusina).

**Kutayarisha dawa ya mimea**

Sehemu za mimea na viungo vyake vyaweza kutumiwa kwa kikamilifu. Waweza kupondaponda sehemu za mimea au miti kisha kuwacha zikae usiku kucha au kuchemsha. Dawa hii hunyunyiziwa mimea au sehemu iliyoadhiriwa na mchwa au wadudu. Vilevile, waweza kutumia sehemu za mmea kama vile maji yatokanayo kwa gome, matunda au machujo na kutumia moja kwa moja.



*Kusiaga au kupondaponda sehemu za mimea ili kutengeneza dawa ya kukabili mchwa.*

*Aina ya mimea iliyo na uwezo wa kukabili mchwa*

| Jamii | Jina la kawaida | Jinzi ya Kuzuia Mchwa | Sehemu zinazozuia |
|---|---|---|---|
| Acacia nilotica | Mtetewa, Mgunga, Mgundi (Egyptian thorn) | Huua | Majimaji |
| Agave americana | (American aloe) | Huchukiza wadudu | Mmea wote |
| Allium sativum | Kitunguu saumu (garlic) | Huchukiza, huzuia, Kukabili vimelea | Mizizi |
| Anacardium occidentale | Mbibo,Mkanju, mkorosho (cashew) | Huangamiza na kuchukiza wadudu | Mafuta ya mbegu |
| Argemone mexicana | (Mexican poppy) | Huua na Kuzuia | Mmea mzima |
| Azadirachta indica | Mkilifi, Mwarubaini, Mwarubaini kamili (neem, nim) | Huua na Kuangamiza mchwa | Majani na mbegu |
| Bidens pilosa | Orogohe (blackjack) | Huua na kukabili | Mmea mzima Mbegu |
| Boswellia dalzielli | Kinondo | Huzuia | Gundi |
| Calotropis gigantea | Mvuzu, Okwot-pu | Huangamiza wadudu | Majani na mbegu |
| Calotropis procera | Mpamba Mrugha Mwitu | Huangamiza mchwa | Gundi |
| Camellia sinensis | (tea) | Huua na kukabili wadudu | Majani |
| Carica papaya | Iripopo, Mpapai,Paipai (pawpaw) | Huchukiza wadudu | Matunda matawi na mbegu |
| Carya ovata | (shagbark hickory) | Huua mchwa | Matawi |
| Cassia siamea | Mbaraka, Msoko (yellow cassia, kassof tree) | Huchukiza kutokana na harufu | Tumia kama boji |
| Cedrela odorata | Mwerezi (West Indian cedar) | Huangamiza mchwa | Mbao |
| Chemopodium ambrosioides | (wormseed) | Huua wadudu | Mmea wote |
| Cleistanthus collinus | Mtazi | Harufu yake huchukiza mchwa | Mgomba |
| Commiphora africana | Mbambara, Mchongoma Mponda, Mturituri, Mtwitwi | Huua wadudu, hasa mchwa | Gundi |
| Consolida regalis | (blue cloud) | Huangamiza mchwa | Mbegu |
| Diospyros ebenum | Lusui, Mdaa-mwitu, Mseseru (ebony) | Hukabili wadudu | Mizizi |
| Hardwickia mannii | | Huua mchwa | Mgomba na matawi |
| Hyptis spicigera | (labiatae) | Harufu yake huchukiza mchwa | Matawi |
| Juniperus virginiana | Murana, Tarakwa (eastern red cedar) | Huangamiza wadudu | |

| Jamii | Jina la kawaida | Jinzi ya Kuzuia Mchwa | Sehemu zinazozuia |
|---|---|---|---|
| Leucaena leucocephala | Lusina, Mlusina (horse tamarind, lead tree, leucaena, white lead-tree, white popinac, wild tamarind) | Huchukiza | Tumia kama boji |
| Melia azedarach | Mmelia, Mwarubaini nusu (chinaberry, persian lilac) | Huua na kuangamiza wadudu kutokana na sumu yake | Matawi, mbegu na Maji ya matunda |
| Mesna ferrea | | Huua wadudu | |
| Ocimum basilicum | Vumba manga (sweet basil) | Huangamiza na kuua wadudu | Mmea wote |
| Ocimum canum | Murumbawasi (wild basil) | Huchukiza na kuangamiza wadudu | Mmea wote |
| Ocimum urticifolium | Makoli (basil) | | Majimaji |
| Pinus strobus | | Huua mchwa | Migomba |
| Prosopis africana | | Huua wadudu | Mizizi |
| Quassia indica | | Huua mchwa | Majani |
| Quercus prinus | (chestnut oak) | Huua mchwa | Maganda |
| Samadera indica | | Huua mchwa | Majani |
| Santalum album | (sandalwood) | Hukabili wadudu | |
| Sassafras albidium | | Huua mchwa | Maganda |
| Semecarpus anacardium | | Hukabili wadudu | Mbegu |
| Swartzia madagascariensis | | Huchukiza | Fruit |
| Tagetes minuta | Tururu (Mexican marigold) | Harufu yake huchukiza wadudu | Majimaji |
| Tectona grandis | Msaji, Mtiki (teak) | Hukabili wadudu | Majimaji |

**Marejeleo**

**"Organic Termite control"** (1994) P Forshaw, HDRA undergraduate report.

**"Natural pest and Disease control"** (undated) H Elwell and A Mass, published by the natural Farming Network, P.O Box 8515, Causeway, Harare, Zimbabwe.

**"Natural pest and Disease control"** (1996) Gaby stoll, published by Magraf Verlag, P.O Box 105 97985 Weikersheim, Germany.

Maelezo ya ziada kuhusu; Viunga vya miche, Mboji ya Kijani, Kuzuia kwekwe, Miti yenye manufaa kama vile Mwarobaini na Mzunze, Kilimo Hai, na jinsi ya kukabili Magonjwa na wadudu yanaweza kupatikana kutoka HDRA:

The Organic Advisory Service
HDRA – International Development Programme
Ryton Organic Gardens
Coventry CV8 3LG
UK
Simu: +44 (0)24 7630 3517
Kipepesi: +44 (0)24 76623 9229
Barua-pepe: ove-enquiry@hdra.org.uk
Mtandao: www.gardenorganic.org.uk/international_programme/

Madhumuni ya shirika la HDRA ni kufanya utafiti, kutoa na kueneza habari kuhusu Kilimo Hai, Ukulima na chakula katika Uingereza (UK) na Dunia nzima. Mwongo mmoja uliopita, shirika hili limekuwa likisaidia katika kubuni njia za kuboresha na kutafiti aina ya ukulima hasa Kilimo Hai katika nchi za hari (Tropics). Vilevile kutoa maelezo na majarida kuhusu Kilimo Hai na pia kutoa mbegu na maelezo ya upanzi.

Maelezo haya yanaweza kunakiliwa bure kwa njia yoyote pasipo malipo.

Tafsiri na:
Patrick Bunyali Kamoyani, P.O Box 1, 50321-Magada via Maragoli, Kenya.
pbkamoyani@excite.com

Kimehaririwa na Leonard Mtama

HD
RA

©2006 HDRA Publishing